A2

Namba ya utambulisho 9222
Majina yangu matatu Kamili Kama yalivyo Sajiliwa Shuleni FLORENT ADAM FLORENT
PREM 20205833471
Ni Mwanafunzi wa kidato cha VI Katika Shule ya sekondari Kagango

Jina la mzazi na namba yake ya simu
ADAM FLORENT HELMAN NO 0684388301

Anuani ya posta
Shule ya Sekondari Kagango,
S.L.P 62,
BIHARAMULO.

Shule anayosoma halimashauri na mkoa Shule
KAGANGO
Halimashauri Biharamulo
Mkoa Kagera

Jina na namba ya simu ya mkuu wa Shule TUMAINI FRANCE 0755180620.

THE HEADMASTER
KAGANGO SECONDARY SCHOOL
P.O.Box 62- BIHARAMULO

## MAENDELEO YA TANZANIA BAADA YA UHURU

Uhuru ni hali ya mtu au kundi la watu fulani kujiongoza aidha kimawazo au kimaamuzi katika katika nyanja zote yaani kiuchumi, kisiasa au kiuchumi, pia kundi hilo laweza kuwa wilaya, mkoa au taifa kwa ujumla.

Tanzania ilipata uhuru wake mwaka 1961 desemba 09 kutoka katika mabavu ya muingereza ambapo uhuru huo ulipatikana pasipo kumwaga damu ya mtanganyika. Hivyo yote ni kutokana na busara za viongozi wapigania uhuru wakiongozwa na hayati baba wa taifa mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Muda mfupi tu baada ya uhuru ndipo ikazaliwa Tanzania kutokana na muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964, Aprili.

Jitihada za viongozi wapigania uhuru ilikuwa ni kuwataka watanzania wajijenge nchi yao pasipokuwa chini ya taifa lolote. Hivyo yapo mambo makubwa ya kimaendeleo yamefanyika baada ya uhuru. Yaani Tanzania imeendelea kisiasa, kijamii na kiuchumi pia. Hivyo maendeleo hayo yameonekana kama ifuatavyo;

Kuanzishwa kwa katiba ya nchi, baada ya uhuru 1961 Tanganyika ilipewa katiba ambayo ilimuhusisha malikia elizabeth kama kiongozi wa juu zaidi akifuatiwa na waziri mkuu Julius K. Nyerere. Ilipofika mwaka 1962 Tanganyika ikaundwa katiba ya kijamhuri ambayo ilimtoa malikia na kumweka rais kama kiongozi wa juu zaidi wa serikali, pia mwaka 1964 kulifanyika mabadiliko ya kikatiba na kuundwa kwa katiba ya muungano. Hata hivyo mnamo mwaka 1977

A2

ndipo mabadiliko mengine yalifanyika na kuundwa au kupata katiba ya kudumu ambayo ndiyo inatumika mpaka hivi sasa.

Kuanzishwa kwa tume huru ya uchaguzi, mnamo mwaka 1995 Tanzania bara iliunda tume ya uchaguzi ambayo ilikua inasimamia na kutangaza matokeo kwa wananchi baada ya uchaguzi. Mfano mnamo mwaka 1995, 2000, 2005, 2010, 2015 na 2020. Tume imeweza kutangaza matokeo halali ya mgombea aliyeshinda kwenye uchaguzi mkuu, vilevile tume imesaidia kuleta amani nchini Tanzania bara. Hivyo basi tume chanzo cha kuimarisha haki na usawa katika suala la uchaguzi nchini Tanzania.

Azimio la Arusha (1967), ni mkutano uliofanyika mjini Arusha Tanzania bara kwa lengo la kuinua uchumi wa nchi ambapo mikakati mingi ilianzishwa mfano, elimu ya kujitegemea, kuanzishwa kwa vijiji vya ujamaa (ujamaa policy), utaifishaji ambapo Mwalimu Nyerere alikuwa mwenyekiti wa mkutano huo. Ambapo vijana walihamasishwa kufanya kazi kwa bidii na kushirikiana, hivyo basi maendeleo ya nchi yalikuwa kupanda kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kutengenezwa na kuboreshwa kwa miundombinu, baada ya uhuru Tanzania bara imeweza kupata maendeleo kama vile barabara, reli, madaraja na majengo, ambayo yamekuwa yakisaidia shughuli za kimaendeleo. Ambapo mwanzoni ilikuwa dhaifu na kutokuwepo kabisa, mfano ya miundombinu hiyo ni kama Reli ya TAZARA, Daraja la Kigamboni, Daraja la Busisi, Reli ya kisasa ambayo bado inajengwa.

A2

Maendeleo katika viwanda, katika miaka 60 ya uhuru Tanzania bara imefanikiwa kujenga na kuboresha viwanda ambavyo vinasaidia katika kukuza maendeleo ya nchi ambapo watu wengi wameweza kupata ajira na kuongezeka kwa masoko ya bidhaa za ndani ya nchi, mfano wa viwanda ni kama kiwanda cha nguo cha mwanza, urafiki Dar es Salaam, viwanda vya sukari vya mtibwa na Kagera. Vilevile serikali imeweza kuhamasisha watu katika shughuli za viwanda nchini kwa kutumia misemo kama HAPA KAZI TU, TANZANIA YA VIWANDA.

Maendeleo katika usafirishaji na mawasiliano, baada ya uhuru Tanzania bara imefanikiwa kununua ndege, meli, treni, magari ya serikali kama UDA ambayo yanasaidia katika kuleta maendeleo nchini katika kusafirisha bidhaa, madini, wafanyakazi kutoka sehemu moja hadi nyingine. Vilevile katika upande wa mawasiliano Tanzania bara ilianzisha TCRA ambacho kimeweza kujenga mahusiano mazuri na mashirika binafsi ya Runinga, Radio, Barua pepe na hata katika simu za mikononi mfano Tigo, TTCL Airtel na Vodacom. Ambapo huduma hizo zimepelekea kukua kwa uchumi na mahusiano mazuri katika serikali.

Kudumisha utamaduni wetu, katika miaka 60 ya uhuru Tanzania bara imeweza kuongeza uthamani wa ngoma zetu za asili na tamaduni zetu kwa kuanzisha Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA) ambalo limesimamia utamaduni wetu. Vilevile Tanzania bara imeweza kuhamasisha michezo kwa wanafunzi na vijana kwa kuanzisha UMISETA kwa wanafunzi wa sekondari na UMITASHUMITA kwa wanafunzi wa

A2

Shule za msingi na pia kuanzishwa kwa timu za Vijana chini ya umri wa miaka 20 kama SERENGETI BOYS na NGORONGORO HEROS.

Maendeleo katika idara ya afya, baada ya uhuru Tanzania bara imeweza kufanikiwa katika elimu bora kwa kubadilisha na kuboresha huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga vituo mbalimbali vya afya nchini na hospitali ambavyo vimeweza kuchangia kupunguza vifo chini pia kuongeza vifaa vya afya kama vile x-rays, madawa, vifaa vingine. Vile vile Tanzania bara imeweza kupambana na magonjwa hatarishi kama vile malaria, Ukimwi, Kipindupindu, Kifua kikuu, Ebola na virusi vya corona 2019.

Hivyo basi, kutokana na mafanikio ambayo Tanzania bara imepata, pia kuna changamoto zimekuwa zikirudisha maendeleo nyuma mfano njaa kali ya mwaka 1973, vita vya Kagera, Rushwa, madawa ya kulevya, kukua na Sayansi na teknolojia duni na udhaifu katika kusimamia miradi ya kimaendeleo. Tunashauri uongozi na wananchi kuwa wajibikaji katika maeneo yao ya kazi ili kuleta maendeleo zaidi nchini Tanzania bara.